Queensland Government

mhrt
Mental Health Review Tribunal

# Kitu gani cha kutarajia kwenye Mahakama ya Pitio ya Afya ya Akili

## Nini maana ya mahakama ya MHRT?

Mahakama ya Pitio ya Afya ya Akili (pia inajulikana kama **Mahakama** au **MHRT**) ni kitengo cha kujitegemea cha kufanya maamuzi. Siyo sehemu ya huduma ya afya au timu ya matibabu.

Kwenye kesi ya MHRT, MHRT itafanya maamuzi kuhusu mamlaka/amri lako la kutokulazimishwa. Watu wanaofanya maamuzi wanaitwa wanachama. Wanachama wanaweza kuwa wanasheria, madaktari au wana jamii. Mwana jamii ni mtu ambaye siye daktari au mwanasheria ambaye ana uzoefu unaostahili kuweza kufanya maamuzi.

MHRT inasikiliza habari kutoka kwako na timu yako ya matibabu. MHRT inaamua:

1. Uwe unataka au hautaki kukaa kwenye mamlaka/amri; na
2. pale unapopokea matibabu na/au matunzo(k.v kama unataka kukaa kwenye hostipali kama mgojwa wa ndani).

kwa wale ambao wako kwenye amri ya matatizo ya akili, MHRT kwa kawaida itaamua:

1. kwa wagojwa hospitali, ni kiasi gani cha likizo kwenye jamii wanaweza kuwanayo; na
2. mazingira ya kwenya amri (k.v. kitu gani mtu anaweza kufanya na kipi hawezi kufanya).

MHRT haiwezi kufanya maamuzi kuhusu matibabu yako au kiasi cha dawa.

## Nitajuaje ni lini kesi yangu itasikilizwa na je nalazimika kwenda?

Utapokea ujumbe kwenye posta ambao utakwambia ni lini kesi itasikilizwa na wapi itafanyikia.

Kesi mara nyingi hufanyikia kwenye hospitali yako ya mahali au kituo cha afya ya akili cha mahali. Kesi yako inaweza kufanyika macho kwa macho au kwenye simu au kwenye mkutano wa video. Kama ungependa kuhudhuria kwa simu au mkutano wa video, tafadhali wasiliana na MHRT.

Hulazimiki kwenda kwenye kesi, lakini ni mda mzuri kwako kuweza kusema utakavyo. Haulazimishwi kwenda kwenye kesi peke yako. Unaweza kuchukua mlezi, ndugu wa familia au rafiki kuweza kukusaidia. Kama hauwezi kufika kwenye kesi, bado unaweza kutoa maoni yako kwa MHRT kupiti fomu ripoti binafsi au kwa kutuma barua pepe au barua kwa MHRT. Kama huwezi kwenda kwenye kesi, MHRT bado wanaweza kufanya maamuzi.

## Naweza kufanya nini kabla ya kesi?

Kama ungependa kuandika ripoti ya kibinafsi, unalazimika kuijaza kabla ya kesi kusikilizwa. Nakala itatumwa kwako kwa posta kabla ya kusikiliza kesi. Unaweza kupata msaada wa kujaza fomu hii kutoka kwa mlezi wako, familia au rafiki. Unaweza kutuma fomu hii kwa MHRT kabla ya siku ya kesi kusikilizwa au kuwapa siku hiyo hiyo.

Timu ya matibabu italazimika kuandika ripoti kuhusu ugojwa wako/ulemavu na maendeleo Wanalazimika kukupa nakala walau siku 7 kabla ya kusikilizwa kesi. Unalazimika kusoma hii na kama una swali lolote unaweza kuuliza timu ya matibabu. Unaweza pia kutoa maoni kwenye ripoti yako binafsi. Unaweza kupata msaada wa kusoma ripoti hii kutoka kwa mlezi wako, familia au marafiki.

Unaweza kupenda kuzungumza na mtu anayekusaidia uliyependekeza au watu wengine wenye uhusiano nawe kuhusu kuhudhuria kesi pamoja nawe. Unaweza pia kupenda kuandaa mwanasheria wa kukuwakilisha, japo hii haitakiwi. Katika baadhi ya mazingira MHRT itachagua mwanasheria kwa ajiri yako Kama iko hivo, mwanasheria atawasiliana na wewe moja kwa moja. Kwa habari zaidi kuhusu mwakilishi kwenye kesi yako, tembelea tovuti ya MHRT au uulize timuya matibabu

## Inatokea nini kwenye kusikiliza kesi?

Kwenye kesi ya MHRT siyo kama mahakama kabisa. Kwa sehemu kubwa utakuwa umekaa kuzunguka meza katika chumba cha mkutano.

Kwenye kesi kutakuwa na watu wawili na wanachama wanne wa MHRT pamoja na watu kutoka timu yako ya matibabu. Unaweza pia kuwa na mtu wa kukusaidia na mwakilishi wanasheria. Wanachama wa MHRT wataweza kuwa kwenye chumba pamoja nawe au wanaweza kujiunga na mahojiano kwenye simu au kwa video. Kama uko kwenye kesi kwa amri ya kutokuwa na akili timamu au mapitio ya hukumu ya kutokuwa vizuri kiakili, mwakilishi wa ofisi ya Mwanasheria Mkuu atahudhuria; kazi zao ni kuwakilisha matakwa ya jamii.

Mambo ya kesi ni ya kibinafsi, hivyo ambao hawahusiki katika matibabu, matunzo au msaada hawawezi kuwa kwenye chumba.

Wanachama watajitambulisha wenyewe kwako ili uweze kujua majina ya kuwaita. Hakuna haja ya kutumia majina ya kiutaratibu kama vile " Heshima Yako".

Wanachama wa MHRT watazungumza na wewe, msaidizi wako na timu ya matibabu kwa kuuliza maswali kuhusu jinsi unavyoendelea. Utapewa mda wote nafasi ya kuwambia wanachama mawazo yako. Unaweza kupenda kuzungumza nao moja kwa moja, kupitia mwakilishi wako au njia zote. Timu yako ya matibabu wataulizwa kutoa maoni yao juu ya maendeleo yako, matibabu na mahitaji ya matunzo na kuimarika.

Wanachama wa MHRT wanaweza kukuuliza wewe, timu ya matibabu na watu wengine kuondoka chumbani kwa mda mfupi wakati wanafanya maamuzi. Wewe pamoja na waalikwa wengine wataitwa kurudi ndani kwenye chumba cha mkutano. MHRT wanaweza kukwambia maamuzi yao au wanaweza kuaamua kukwambia maamuzi mda mwingine. Kwa njia yoyote, maamuzi katika maandishi yataweza kutomwa kwa barua ndani ya siku saba.

## Inatokea nini kwenye kusikiliza kesi?

Unaweza kuomba maelezo ya kimaandishi kuhusiana na sababu za maamuzi yaliyotolewa. Jinsi ya kufanya hivyo imeandikwa katika habari ambazo zitatumwa kwako za maamuzi au unaweza kuwasiliana na MHRT moja kwa moja.

Unaweza kuwa na haki ya kupinga maamuzi yaliyofanywa na MHRT kwenye mahakama ya Afya ya Akili ndani ya siku 60 za kufanywa kwa maamuzi. Habari zaidi kuhusu hili zinaweza kupatikana kupitia Kumbukumbu ya Mahakama ya Afya ya Akili kwa (07) 3082 0554 au kwa barua pepe registrarmhc@health.qld.gov.au

## Habari zinazo husiana na kuruhusiwa hospitali

Kwa habari zaidi kuhusu MHRT, tafadhali tazama tovuti ya MHRT: www.mhrt.qld.gov.au

(07) 3338 8300 / enquiry@mhrt.qld.gov.au